Kwako bibi

Mundere hayupo tena kiongozi wa APHILMA/Bukavu
Amekombolewa na Chibi Cha Bene

Habari kamili kutoka Nyofu kunako makao ya Prezidenti wa Chama jimboni aliye pia Liwali wa jimbo la Kivu zaeleza kuwa mke wake akina mama Mwando Museng Rov, kiongozi wa kamati ya wamama inayohusika na kusaidia wamaskini pamoja na wale wasiojiweza kwa kifupi cha kifaransa "APHILMA" anatoka kuachisha kazi kamati ya kiungo hicho ya hapa Bukavu. Kamati hiyo ilikuwa ikiongozwa hapo awali na akina mama Mundere. Kufuatana na habari tulizopata, inaaminika kuwa mama Mundere pamoja na wasaidizi wake walionekana kuwa wabovu katika kazi walizopewa na hawakuweza kushikilia vema mipango ya kuendelesha kamati yao. Muda wa siku zote walizotumikia kamati hiyo, walifanya tu vitendo viwili vinavyostahili sifa. Waliweza tu kuwasaidia wamaskini na mkoa wa Nguba na kuwatolea dawa wagonjwa wa hospitali ya hapa Bukavu.

Mama Mwando Museng Rov alishikwa na hasira na akachukua hatua ya kuangusha kamati ya mama Mundere na kuikomboa na ile itakayoendeshwa na akina mama Nkubonage Chibi Cha Bene ambaye pia ni kiongozi wa shirika la wafanya biashara wa hapa Bukavu. Kufuatana na kutajwa kwake huko kama vile mkurugenzi wa APHILMA/Bukavu, mama Chibi cha Bene aendelea kupokea barua za kumpongeza na kumtakia maendeleo mema katika kazi yake hiyo. Kamati ya APHILMA/Bukavu yapangwa namna ifuatayo : Prezidenti: Chibi cha Bene akisaidiwa na Mahamba pamoja na Bunzigiye. Katibu ni daktari Nzuzi. Mlinda feza: Mama Litanda na makamu wake ni mama Mwambali. Mama Mwando alisifu sana kamati ya APHILMA ya wilaya ya Kivu la Kusini. Wanamemba wake wamekwisha kupata mavazi pamoja na vyeti vya kuwatambulisha.

Mnamo siku zilizopita, mama Mwando alimuonya kiserikali kwa wake wa viongozi mbali mbali katika Chama na serikalini, mke wa makamu wa liwali wa jimbo anayejulikana kwa jina la Koyagialo. Sherehe hizo za shangwe ziliendeshwa kunako makao ya liwali pa Nyofu. Kila mara kunapopatikana mgeni miongoni mwao, wamama hao wazoea kukutana katika sherehe za namna hiyo kusudi wapate kuelewana na kusikiliza mashauri mema ya mke wa liwali wa jimbo, akina mama Mwando Museng Rov.

Kaboyi Habimana.

Kivu ya Kusini

Burhinyi : Mwami Muganga ajiuzulu

Habari zinazoaminika toka Kivu ya Kusini na zilizotolewa na mwaandishi wetu Musemi Kilondo Nkula anayehusika na kituo chetu cha habari wilayani humo zahakikisha kuwa Mwami Muganga Basengezi aliye pia kiongozi wa asili wa mkoa wa Burhinyi katika mtaa wa Mwenga aliweza kujiuzulu na kuachia kiti chake cha ezi mtoto wake LUMA Basengezi.

Kujiuzulu kwa Mwami Muganga kwatokana na ugomvi unaofanyika siku kwa siku kati ya Mwami huyo na kiongozi wa mkoa mdogo Bugoye aliye pia mjomba wake. Akimwaachia mtoto wake Luma kiti cha ezi kwaleta jawabu kwa magumu na matatizo yaliyokuwa yakiwasonga wakaaji wa mikoa huo.

Kwa kweli yasemekana kuwa kuchaguliwa kwa kijana Luma kwatokana na masimulizi rasmi Mwami Muganga aliyoyafanya na wazee wa baraza lake "bajinji" ambao walinda mila na desturi za asili za mkoa. Kiongozi huo wa sasa ana umri wa miaka 25 na ni mtoto wa nne wa Mwami Muganga aliyechaguliwa kati ya ndugu zake 22. Kuchaguliwa kwa kijana huyo kulishangiliwa na umati wa watu na wakaaji waliokuja kuzuria mkusanyo huo uliofanyika chini ya uongozi wa mwenyekiti wa wilaya wa Kivu ya Kusini, mwananchi Mandokoma-Bongoy. Hata mwananchi Bugoye aliye mpinzani wa Mwami Muganga naye pia alifurahiwa na uchaguzi huo.

Kwa sasa mkoa wa Burhinyi waongozwa bado na mwananchi Mutuzi Civarara aliye makamu wa prezidenti wa shauri la mkoa. Madaraka hayo aliyakabizwa na mwananchi Luma Muganga aliye kiongozi wa asili, mwami wa mkoa wa Burhinyi kwa sasa na prezidenti wa shauri la baraza la mkoa akigonjea hivi kusimikwa kiserikali.

Itajulishwa hapa kuwa ni tangu mwaka wa 1955 Mwami Muganga aongoza mkoa huo baada ya kuachiwa uongozi wa mkoa na mjomba wake Bugoye alipokuwa bado mdogo. Ila kisha miaka michache mwananchi Bugoye alimshtaki mpwa wake yakuwa awaangamiza wakaaji akiwanyanganya mali zao, katenda maovu mengi na kazalika kwa kuwasonga na kuwagandamiza.

Twazani kisha kuchaguliwa kwa Mwami Luma Basengezi kutaleta masikilizano kati ya jamaa hizo mbili na hasa kati ya wakaaji na viongozi wao.

Bisimwa L-B. Tserou.

JUA

Gazeti la Kivu

Mwaka wa 12 n° 287 Tarehe 9 mpaka 15 Novemba 1985

Kiongozi : Mutiri-wa-Bashara

HABARI ZA POPOTE

Kivu

Vilalo vya Fizi vitatengenezwa

Aliporejea Bukavu kiisha juma yapata tatu ya kazi pale Kinshasa, mji mkuu wa Taifa letu, liwali wa jimbo la kivu, mwananchi Mwando Nsimba alitolea hapa majuzi wasaidizi wake ripoti kamili ya safari yake.

Katika mkusanyo wa kamati ya Chama (Comité Central) ya kuimarisha Chama chetu cha mapinduzi ambacho kinafanya fungo moja na nchi yetu Zaïre.

Kwa hiyo, imekumbushwa kwa kila mzairwa kama yeye ni mwanamapinduzi anayepashwa kuishi kimapinduzi na kutoa nje wote warugaruga wanaotutakia magumu.

Akifasiria matatizo ya jimbo letu, liwali Mwando alitoa mwanga kuhusu mazungumzo alioifanya na wakuu wa nchi. Ni hivi tarehe 18 Novemba, atajielekeza katika mkoa wa Fizi ambako atatia jiwe la kutengeneza vilalo juu ya mito Sandja na Kibumba. Vilalo hivyo vitatengenezwa binafsi na Ofisi ya mabarabara nchini (Office des Routes).

Kuhusu kazi zingine, Benki kuu Ulimwenguni iliitika kutoa kiasi cha feza za kutosha kwa kukomesha miporomoko ya udongo ya Funu na Baraza ya mawaziri itachungua jambo la utengenezaji wa mabarabara mikoani.

Juu ya majengo isiyo halali, Kamati ya Chama imempa makamu wa liwali wa jimbo madaraka ya kuchungua vema jambo hili kwa ginsi ya kuazibu vikali mtu yeyote aliye jiruhusu kujenga ovyo ovyo ama kuruhusu majengo hiyo.

Kufuatana na ukosefu wa mafuta ya taa na yale ya kutembeza gari, kamati ya Chama jimboni imekubalia wafanyabiashara wenyi kujiweza kununua na kuuza mafuta hayo jimboni mwa Kivu.

Mwalimu Ali Mwinyi ndiye kiongozi mpya wa Tanzania

Habari zinazoaminikiwa kutoka Dar es-Salam zatupasha kwamba tangu tarehe 6 mwezi huu wa Novemba Tanzania ina kichwani mwake kiongozi mpya aitwaye Mwalimu Ali Mwinyi.

Prezidenti huyu amkomboa mzee Julius Nyerere Kambarage aliyeamua tangu mwaka moja sasa kupumzika kisha miaka 23 ya uongozaji wa nchi. Wasomaji wetu wataelewa kwamba Mheshimiwa Mwinyi alitajwa na Prezidenti Nyerere peke yake mbele ya kuchaguliwa na raia waliyomuitika kwa kumpatia sauti 99 juu ya mia.

Kwa ngambo ingine, imesemeka huko Dar es-Salaam kama ingawa Mwalimu mkuu ameacha kiti cha prezidenti, atabaki na cheo chake cha katibu mkuu wa CCM (Chama Cha Mapinduzi) ya Tanzania ambacho aliunda peke yake.

Kwa kumaliza, Nyerere ndie Presidenti wa tatu katika bara la Afrika anayejejiuzulu peke yake bila wasiwasi. Wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Léopold Sedar Senghor alifuatwa na wenzake Ahmadou Ahidjo wa Cameroun, Jerry Rawlings wa Ghana ambaye alirudilia mara pili kiti cha Prezidenti.

Kajangu Mususu.

Shairi

Bora uzima

Mama nakufa
Nini mtoto nini ?
Njaa, tumbo nauma.

Taratibu mtoto
Nami bado sikula
Tumboni hamna kitu
Ingawa mama ni mimi !

Unawazaje sasa ?
Mimi siwazi najua
Njaa imezidi
Na pesa hatuna.

Tutakufa mbone !
Hiyo hapana jua
Mola tasaidia
Yote utashi wake.

Kwa nini kunizaa basi
Wewe na mimi njaa
Sio peke yetu
Kote duniani huteswa.

Na si njaa tu
Kuna pia ugonjwa
Vita, miporomoko
Mitetemeko ya ardhi
Mukunguru, misiba
Na vinginepo.

Watu huteketea
Hufa na kuumia vikali
Ole kwao kweli
Kwani heri tena njaa
Isingeua mtu !

Tangolek.

Je Umesikia...?

KWAMBA kuna jamaa wanalo wazo la kusema kuwa kutwangana makonde (ngumi) ndiyo kujipatia sheria? Hapo majuzi walimu wawili wa masomo ya ufundi walitwangana makonde katika ofisi ya mkurugenzi wao. Chanzo cha ugonvi huo ni kuona mmoja wao anamshtaki mwenzie katika harakati harakati zake za kuomba wazazi rushwa (kituliro) eti ataandikisha watoto shuleni.

Aliposikia mashtaki hayo, ndipo alishikwa na hasira na akamrukia mwenzie na kuanza kumsakata makonde, makofi na vipasi. Mkurugenzi wa masomo alibaki kinywa wazi na tunangoja hatua atakayoshika mbele ya walimu wake hao wawili.